GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

Mapenzi Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. 237 **Ath Than-Al Ula** 1445 **AH** **NOVEMBA–** 2023 **ZAHOOR** 1402 **HS** **BEI TSH 800/=**

>UK .4 **Yesu aliongozwa na nani Nyikani?**

Ujumbe wa Hadhrat Khalifatul Masih Vatba

Jalsa Salana ya 52 Tanzania - 2023

Ndugu Wanajumiya wa Ahmadiyya Muslim Jama'at Tanzania,

Assalaam alaikum warahmatullah wabarakatuh.



Ninayo furaha kubwa kuwa mnafanya Jalsa Salana yenu ya 52 kwenye tarehe 29, 30 Septemba na 1 Oktoba 2023. Ni maombi yangu, Mwenyezi Mungu aibariki Jalsa yenu kwa

UK. 3

mafanikio makubwa na washiriki wote wapate baraka nyingi za kiroho kwa kushiriki katika mkusanyiko huu wa kipekee wa kidini.

Masihi Aliyeahidiwa (as) alitufundisha tusiifikirie Jalsa kuwa ni mkusanyiko wa kawaida kama mikusanyiko mingine, bali alitangaza kwamba hili lilikuwa tukio ambalo liliegemezwa juu ya mpango wa Mungu, kwa ajili ya kueneza Uislamu na kueneza mafundisho sahihi ya Qur'ani Tukufu na mafundisho ya kipenzi chetu Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w.

Masihi Aliyeahidiwa

Njia ya Kulinda Maadili Mema katika Taifa UK. 10

Jalsa Salana-52 Tanzania

Mhe. Doto Mashaka Biteko Naibu Waziri

Mkuu afikiwa na ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya



UK. 5



Njia ya Kulinda Maadili Mema katika Taifa UK. 10

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Jalsa Salana ya 52

Maelezo ya Khalifatul Masih wa v Hazrat Mirza Masroor Ahmad[atba] akizungumza na waliojitolea kuwapokea na kuwahudumia wageni wa Masih aliyeahidiwa[as] katika mkutano wa Jalsal Salana Uingereza 2023 kwamba tuwatumikie wageni hao kwa **TABASAMU** na ujumbe tulio letewa na Mtukufu Khalifa wa kuongeza viwango vyetu vya Taqwa na hivyo kutimiza haki kwa Allah na haki za viumbe wake. Mambo haya mawili yamekuwa Dira iliyotuongoza na kuleta mafanikio makubwa ya Jalsa Salana ya 52 ya Tanzania.

Mafanikio yanayo jitokeza mahali popote zinapofanyika shughuli za jamaat basi elewa fika kuwa mahali hapo wamezingatia na kutekeleza maagizo ya kiongozi wetu mpendwa. Mafanikio yetu, maendeleo yetu na uzima wetu wa kimwili na kiroho yamo katika kutekeleza kauli ya Huzur.

Jambo jingine ambalo tumejifunza ni Umuhimu Mkubwa wa Historia yetu kama hatufahamu tuliko toka hatuwezi kuelewa tunakoelekea. Tulipata burudani kubwa ya kihistoria kutoka kwa muhusika hasa Amir na Mbashiri mkuu wa Ghana Alhaj Sheikh Noor Muhammad Bin Saleh Sahib aliyekuwa mgeni wa heshima katika Jalsa yetu.

Jalsa ilisisimka kwa kusikia jamati ilivyoingia Gold Coast kabla ya 1957 nchi hiyo ilikuwa inaitwa Gold Coast na ilipopata uhuru 1957 ikawa Ghana. Sheikh Muhammad Bin Saleh aliyeeleza tanuru la moto walililopitia waghana katika kukabiliana na mateso lakini watu wakawa imara na uimara huo ndio unaoifanya Ghana ing'are katika Afrika. Sheikh alitukumbusha kuwa hakuna wasiwasi wowote kuwa Islam itashinda na kuitawala Dunia. Ni wakati wa Afrika kwa hivi sasa kueneza Islam ya kweli na Islam hasa ni Ahmadiyya. Hivyo tunao wajibu wa kuwa tayari kujitoa muhanga kwa ajili ya ushindi wa Islam. Siku zote ushindi haupatikani katika Sahani ya Dhahabu lazima watu wawe tayari kutoa jasho. Miaka kumi na tatu ya Mtukufu Mtume Muhammad[saw] katika Makka ilikuwa migumu na mateso makubwa. Maadui hawakupumzika walimfuata Madina na huko mapambano ya kulinda uhuru wa kuabudu yaliendelea. Swali la msingi alilouliza Alhaj Sheikh Muhammad Bin Saleh ni kwa kiasi gani tuko tayari kupambana ili kueneza ukweli alioleta Mtukufu Mtume Muhammad[saw].

Jambo la tatu ambalo tumelipata na tunatakiwa kulizingatia ni kufanya haraka kufanya utafiti na kuandika historia yetu. Yapo mengi ya kufanya na yapo mengi ambayo hatuyafahamu. Wangapi tulikuwa tunajua kuwa mbegu ya Ahmadiyya kanda ya ziwa kumbe ilipandwa na Maulana wetu akina Sheikh Jamil Rahman Rafiq Sahib, Sheikh yusuf Athumani Kambaulaya, Sheikh Ismail Munir. Kumbe yanayo endelea kanda ya ziwa ni ile mbegu iliyopandwa kwa maombi na juhudi za Maulamaa hao. Tumekuwa tukisikia kuwa akina mama ndio waliouza mapambo yao na kujenga msikiti wa Alfazal London na katika mkutano huu tumejifunza kuwa akina Mama wa Tanzania hawako nyuma. Akina Mama fulani wa songea waliuza mapambo yao na kujenga msikiti wa Songea. Akina mama jasiri wa Rufiji walisimama kidete kulinda haki yao ya kuabudu na walikataa kutoka kwa waume zao. Ni historia ya kusisimua na kuonesha kuwa akina mama wanaweza.

Msichana jasiri Fatma Hasani Ali wa ukutini jimbo la Chambane mara baada ya kujiunga na Ahmadiyya alipitia upinzani mkubwa kutoka kwa wazazi lakini alisimama imara na hakutetereka na alipokuja kuchumbiwa alisema sharti la yeye kuolewa ni kwamba huyo muoaji lazima awe Ahmadiyya na ndivyo ilivyokuwa.

Historia ya awali ya Islam imeonesha akina mama walivyoshiriki kikamilifu katika kuihami Islam. kuna hatari ya kujiona mnyonge kama huifahamu historia yako. Tunalo jukumu la kuandika historia ya Ahmadiyya nchini mwetu na kuhakikisha kuwa tumeisoma.



QUR'AN TUKUFU

22. SURA AL-HAJJ

ذٰلِكَ ۚ وَمَنْ يُّعَظِّمْ حُرُمٰتِ اللّٰهِ فَهُوَ خَيْرٌ لَّهٗ عِنْدَ رَبِّهٖ ؕ وَ اُحِلَّتْ لَكُمُ الْاَنْعَامُ اِلَّا مَا يُتْلٰى عَلَيْكُمْ فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْاَوْثَانِ وَاجْتَنِبُوْا قَوْلَ الزُّوْرِ ۙ﴿۳۱﴾

31. Ndivyo hivyo; na anayevitukuza vitu vitakatifu vya Mwenyezi Mungu, basi hiyo ni heri kwake mbele ya Mola wake. Na mmehalalishiwa wanyama isipokuwa wale mnaosomewa; basi jiepusheni na uchafu wa masanamu na jiepusheni na usemi wa uwongo.



NUKUU YA HADITHI

حَدَّثَنَا عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ أَبِي بَكْرَةَ ، عَنْ أَبِيهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ ، قَالَ : قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ : أَكْبَرُ الْكَبَائِرِ الْإِشْرَاكُ بِاللَّهِ ، وَعُقُوقُ الْوَالِدَيْنِ ، وَشَهَادَةُ الزُّورِ ، وَشَهَادَةُ الزُّورِ ، ثَلَاثًا ، أَوْ قَوْلُ الزُّورِ ، فَمَا زَالَ يُكَرِّرُهَا ، حَتَّى قُلْنَا لَيْتَهُ سَكَتَ

Hazrat Abdur Rehman bin Abi Bakrah anasimulia kutoka kwa baba yake r.a. kwamba, Mtume[saw]. alisema: Dhambi kubwa zaidi kuliko madhambi yote ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu, na kuwaasi wazazi, na kutoa ushuhuda wa uwongo na kutoa ushuhuda wa uwongo, akayarudia mara tatu au (alisema) kusema uwongo na aliendelea kuyarudia rudia hayo hata tulisema; laiti angenyamaza.
(SAHIH BUKHARI HADITH NO:6919)



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Hazrat Ahmad a.s. anasema:

" leo hii hali ya dunia imekuwa mbaya zaidi, tukitazama kwa namna yoyote, mashahidi wa uwongo wanaandaliwa, kufungua kesi za uwongo ni kitu chepesi tu, vyeti vya uwongo vinatengenezwa, wakilieleza jambo basi wataeleza kwa kuuficha ukweli, sasa mtu yeyote awaulize wale wasiofahamu haja ya uwepo wa Silsila hii je, hii ndio dini aliyoileta mtume s.a.w.? Mwenyezi Mungu Alitamka, uwongo kuwa uchafu na tujiepushe nayo.

KUMBUKA AKHERA ========== Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema: Ni wajibu kwa watu kukumbuka Akhera. Mtu anapaswa kuogopa kabla adhabu haijafika. Mtu anayeweka macho yake juu ya akhera ana bahati. Tazama jinsi watu wa Nabii Lut (as) na wengine walivyokabiliwa na mwisho wao. Ni muhimu hata kama mtu ni mgumu wa moyo, anapaswa kumwonya na kumfundisha kuwa mnyenyekevu na mpole. Hili ni la lazima kwa jamii yetu zaidi ya wengine wote kwa sababu wanapokea ufahamu mpya katika mambo ya kimungu. Iwapo mtu anadai kwamba amebarikiwa na ufahamu wa kiungu, lakini hawafanyii kazi, basi madai hayo si chochote ila ni kujifakhirisha na kujisifu tu. Kwa hiyo, jumuiya yetu haipaswi kughafilika kwa sababu ya uzembe wa wengine, wala kuruhusu upendo wao kupoa kwa sababu ya ukosefu wa shauku kwa wengine. Mtu huwa na matamanio mengi. Ni nani aliye na ujuzi wa mambo yaliyofichika ya hatima na hukumu? Maisha kamwe hayasogei sambamba na matakwa ya mtu. Tamaa za mtu ni jambo moja, lakini muundo wa hatima na hatima ni tofauti kabisa, na ni jambo hili ambalo

Inshallah toleo lijalo

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Ujumbe wa Hadhrat Khalifatul Masih Vatba Jalsa Salana ya 52 Tanzania - 2023

KUTOKA UK> 1

alisema:

‘Msiuchukulie Mkusanyiko huu kuwa ni sawa na mkusanyiko wowote wa kawaida wa kidunia. Bali suala la jambo hili ni kwamba, limejengwa juu ya uungwaji mkono kamili wa ukweli na uenezaji wa Uislamu. Jiwe la msingi la Jumuiya hii limewekwa na Mungu, Mwenyezi Enzi Mwenyewe na mataifa yametayarishwa ambayo hivi karibuni yatakuja na kujiunga nalo. Hii ni kwa sababu, ni kazi ya Yule Mwenye Nguvu Zote, Ambaye Kwake hakuna lisilowezekana.’

[Ishtihar Disemba 27, 1892, Majmua e Ishtaharat, Jalada 1, uk 361, Toleo la 2019]

Ni muhimu kwamba mnufaike kikamilifu na mwenendo wa Jalsa ili kujifunza jinsi ya kuboresha viwango vyenu vya kiroho na kimaadili, kuwa bora katika kufanya vitendo vya uchamungu na hivyo kupata ukaribu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Jalsa hii iwawezeshe kuzidisha viwango vyenu vya Taqwa, ambayo ni uadilifu, na ifanye hofu ya kweli ya Mwenyezi Mungu ikue ndani ya nyoyo zenu. Hakika lengo lenu pekee liwe ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

Kwa hakika, Masihi Aliyeahidiwa (as) amesema kwamba lengo la kweli la maisha ni sisi kufungua dirisha la mioyo yetu kuelekea kwa Muumba wetu. Anasema:

‘Enyi watu, mmeumbwa kwa ajili ya utambuzi, upendo na utii kwa Muumba wenu wa Kweli na Mungu wenu wa Kweli.’ [Essence of Islam Jal IV uk. 146]

Kwa hivyo, mnapaswa kujenga uhusiano wa kibinafsi na Mwenyezi Mungu Mtukufu, kusali sala zenu tano za kila siku mara kwa mara na kwa jamaa, mzidishe dua zenu na kudumisha kumkumbuka Mwenyezi Mungu daima ndani ya nyoyo zenu.

Ninakunasihini muweke mafungamano madhubuti na Khilafat-e-Ahmadiyya na mtoe shukrani endelevu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutupa matunda yanayoendelea ya taasisi hii yenye baraka. Hatupaswi tu kusali sala za dhati za shukurani kwa Mwenyezi Mungu kwa kutuneemesha kwa baraka nyingi za Ukhalifa, bali pia tunapaswa kuweka kiapo kizito kwamba tutajishughulisha na matendo mema na ya kheri na kujitahidi daima kuwa Waislamu wa Ahmadiyya wa kupigiwa mfano. Kumbukeni, mafanikio yetu yanatokana na kushikilia kamba ya Mwenyezi Mungu na kushikamana na taasisi ya Ukhalifat-e-Ahmadiyya, ambayo inawakilisha Ukhalifa pekee wa kweli na wa haki kwa Waislamu leo. Ni kwa kufuata kwa uaminifu tu mwongozo wa Khalifat-ul-Masih, ndipo mtaweza kuufahamisha ulimwengu kuhusu mafundisho safi na ya kweli ya Uislamu.

Pia ni muhimu daima kuunga mkono na kushirikiana kikamilifu na Nizam e-Jama’at kwa moyo wa utiifu wa kweli, kwa sababu tunaweza tu kusonga mbele na kupiga hatua kama tutaendelea kuwa wamoja, na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya kufikia malengo matukufu ya Jumuiya.

Mnapaswa kutazama MTA mara kwa mara na kuzihimiza familia zenu, hasa watoto wenu, kufanya hivyo pia. Hasa, mnapaswa kusikiliza mara kwa mara hotuba zangu za Ijumaa, na hotuba zangu katika hafla na matukio mengine. Hii itakuwezesheni kudumisha uhusiano wa kudumu na Khilafat na itaimarisha imani yenu. Mnapaswa pia kuzingatia wajibu wenu kuhusu mahubiri ambayo ni muhimu kwa kila Ahmadiyya, na mnapaswa kupanga kwa busara na kubuni njia mpya na za hekima za kueneza ujumbe wa amani wa Islam Ahmadiyyat kote Tanzania na nchi jirani.

Kwa kumalizia, ni dua yangu ya dhati, Mwenyezi Mungu aibariki Jalsa Salana yenu kwa mafanikio makubwa na awawezeshe nyote kuimarisha na kukuza imani yenu. Mwenyezi Mungu akuwezesheni kuleta mabadiliko ya kweli katika maisha yenu kuelekea uchamungu zaidi, tabia njema, matendo mema na huduma ya Islam Ahmadiyyat na ubinadamu.

Mwenyezi Mungu awabariki nyote.

Wassalam

Wenu mwaminifu,

Imesainiwa

MIRZA MASROOR AHMAD

KHALIFATUL MASIH V



Yesu aliongozwa na nani Nyikani?

Kutoka toleo lililopita

(7) KUJITUPA KWA MAKUSUDI KUTOKA JUU YA KINARA.

Kujitupa kwa makusudi kutoka juu ya kinara kutegemea Mungu Atakuokoa, huko nako ni kukosa kutumia AKILI na ujinga uliofurutu ada ambako hakuwezi kufanywa na mwanadamu yeyote mwenye akili timamu.

Kwa maana hiyo ilikuwa anajulishwa hali mbaya ya wafuasi wake watakavyo shindwa kutumia AKILI kuhusu swala linalo husu imani, bali watakuwa radhi kufuata kila wataloambiwa na viongozi wao bila ya kujali madhara yoyote yatakayotokea.

Jambo hili lipo wazi sana kwenye imani ya kikristo. Kwamba wao suala la kutumia akili kwenye mambo ya kiroho, hawana kabisa. Na ndio tunaona leo kwamba hakuna mkristo anayethubutu kupinga kauli ya kiongozi wake wa kanisa.

Kuambiwa YESU ni Mungu asilimia mia moja wao sawa. YESU amelaaniwa na Mungu sawa.

Watu wote wana dhambi ya kurithi kutoka kwa Adam sawa. Ila kila MTU atabeba furushi LA dhambi zake, sawa. YESU hana dhambi, sawa. Yesu amefia msalabani na hivyo amechukua dhambi za watu wote, sawa. YESU yuko hai mbinguni sawa. Hata kama awe msomi kiasi gani, tena awe, profesa, Doctor, mwenye PHD, wote hakuna wa kufurukuta mbele ya mchungaji wake.

Na imani hizo zote zinakataliwa ndani ya Biblia takatifu, Bali anaitwa mjinga mtu wa sampuli hiyo ya kuamini kila jambo bila ya kutafakari.

Anashindwaje kutafakari ilhali amejaaliwa akili? Ama kweli mjinga huamini kila jambo, mithali 14:15--16;

Hata Mungu mwenyewe anasikitika, watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa (AKILI); hoseo 4:6; Na kama hutumii maarifa (AKILI) uliyopewa, Mungu HAKUTAKI na Yesu pia hakutaki. Kwa ushahidi wa maneno haya ya Yesu:-

Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba;

mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba.

Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga;

mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa. (Mathayo 27—7:24)

(8) KUONESHWA MILKI YA DUNIA NA SHETANI ILI ASUJUDIWE ANGALAU MARA MOJA TU ILI APEWE.

Kwa mujibu wa maandiko kusujudia kitu chochote kiwe baharini au ardhini au mbinguni kumekatazwa vikali sana na Mungu mwenyewe.

Kwa maana hiyo njozi iliendelea kumjulisha Yesu wafuasi wake jinsi watakavyo shindwa kufuata mafundisho sahihi ya MUNGU na kuiangukia DUNIA, na unapoisoma historia ya ukristo hasa kanisa la Romani Katholiki inasikitisha sana, au kitabu kilichotungwa na Bw, Ellen G.white, kiitwacho, TUMAINI KUU, inasikitisha na inaleta huruma.

Watu hao wanajitangaza kuwa wanasimamia amani ya Yesu.

Na kwa wale waliojalibu kupinga mapokeo ya kanisa na mauzo ya vyeti vya toba ili wapate ufalme wa Mungu.

walikuwa wanapata mateso makali sana na hatimaye kuwasababishia vifo, na ukisoma mafundisho ya Yesu, anasema wasichukuwe chochote wamepata bure watowe bure. Mathayo 10:9

(9) KUTIMIA KWA NJOZI YAKE JUU YA KUACHWA KWA MAFUNDISHO YAKE.

Mwenyezi Mungu anapotuma watumishi wake huwa anawasiliana nao kwa kuwapa taarifa mbalimbali na mutukio yatakayo tokea baadae ili ukweli wake uthibitike.

Kwa kauli ya Yesu mwenyewe Ametaja makusudio ya kuja kwake na katika makusudio hayo mojawapo ni kusimamia sheria ya Musa na kauli za MANABII waliomtangulia.

«Sikuja kuitangua torati au manabii la; bali kutimiliza kwa maana amini nawaambia mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka yodi moja; wala nukta moja ya torati haitoondoka hata yote yatimie

Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo na kuwafundisha watu hivyo ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni,

Bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni. (Mathayo 5:17--19;)

Pia kisipunguzwe wala kuongezwa chochote katika kitabu hiki.

Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu yeyote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki, Na mtu yeyote akiondoa lolote katika maneno ya unabii wa hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa

uzima na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki. (Ufunuo 19—22:18)

Hata yule kijana tajiri alipomuuliza mwalimu wake afanye nini apate ufalme wa Mungu alimwelekeza kwenye taurati. Mathayo 19:16--22;

Mwanafunzi awe Kama mwalimu wake Mathayo 10:24--25; na wasichukuwe chochote . Mathayo 10:9--10;

Lakini mafundisho hayo ya Yesu ukiyalinganisha na vile walivyofundisha na wavyoendelea kufundisha Wafuasi wake, unakuta ni tofauti kabisa. Na huko ndiko kutimia kwa yote yaliyoelezwa kwenye njozi ile iliyosimuliwa katika Mathayo 11-4:1.

Wafuasi wa Yesu Sheria kwao ni laana Wagalatia 2:16--21 na wagalatia 3:10--13;

Agano la kutahiriwa kwao halina umuhimu. Wagalatia 5:2--6.

Katazo la kutowaendea watu wa mataifa mengine wamelivunjilia mbali. (Mathayo 10:5; 10:23;

Tena kwa kufunga midomo ya wenye hoja mmoja wao akazua kuwa amepewa Injili ya watu wasiotahiriwa yaani ruhusa ya kuwahubiria Injili watu wote duniani imetolewa. Wagalatia 2:7.

Matendo 14:27.

(10) MTI UTAUTAMBUA KWA MATUNDA YAKE

NA UNAFIKI HAUTAKIWI KATIKA DINI NI UKAFIRI.

Akaona mtini mmoja kando ya njia, akauendea, asione kitu juu yake ila majani tu; akauambia, Yasipatikane matunda kwako tangu leo hata milele. Mtini ukanyauka mara. Mathayo 21:19.

Huu ni msemo wa kimafumbo ambao unaeleza jinsi Yesu alivyo walaani wana wa Israeli.

kustawi majani tu, maana yake ni kuipenda dunia tu,(maisha ya dunia), mioyoni mwao mmejaa uasi mtupu.

Na ndio maana Yesu aliwahi kusema "Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa ngozi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali, mtawatambua kwa MATUNDA yao, Je! watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika mibaruti? Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; Na mti mwovu huzaa matunda mabaya.

Mti mwema huwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu huwezi kuzaa matunda mazuri. Kila mti usiozaa tunda zuri hukatwa ukatupwa motoni. Ndiposa kwa MATUNDA yao mtawatambua. (Mathayo —7:15 20)

Na YUDA akasema

Wapenzi, nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, na kuona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie IMANI waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.

Kwa maana kuna watu waliojiingiza kwa siri, watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, MAKAFIRI, wabadilio neema ya MUNGU wetu kuwa ufisadi, nao humkana yeye aliye peke yake Mola, na Bwana wetu YESU kristo. Yuda 1:3--4; (Mungu ni mmoja tu.);

Kuna watu wanaingia kwenye dini kwa lengo la kuvuruga ukweli ili wamkatae Mungu wa kweli na Mtume wake, huwa wanatambulika kwa vitendo vyao na ndio maana Mungu anasikitika WATU wake wanaangamizwa kwa kukosa maarifa (AKILI,); Na yeye hawataki wasio tumia akili.(Hosea 4:6)

YESU mwenyewe hakuruhusu mchanganyiko katika mambo ya IMANI.

Mwanafunzi mmoja alimuomba ruhusa mwalimu wake akamzike Baba yake hakupewa nafasi hiyo alichoambiwa waacha wafu wazike wafu wao. (Mathayo 8:21--22)

Huyo ni Baba yake sembuse kabila jingine,

jifunze jambo hapo aliyekufa (maiti) atawezaje kumzika mwenzie. !! ??; kwa maana hiyo Baba yake kwa kukosa kuyajuwa mafundisho ya MUNGU kiistilahi ya dini mtu huyo amaitwa mfu. (UMEKUFA).

HIKI NI KIKOSI KAZI CHA WANAFIKI WALIOWAPOTEZA WATU NA KUIACHA IMANI SAHIHI ILIYOFUNDISHWA NA YESU.

(1) Yuda Iskariote

(2) Petro wa (kefa);

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Mhe. Doto Mashaka Biteko Naibu Waziri Mkuu afikiwa na ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya

Kutoka Uk> 1

Mnamo tarehe 18 Sep 2023 ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Tanzania ukiongozwa na Amiri na Mbashiri Mkuu Tanzania Maulana Tahir Mahmood Choudhry Sahib ulifanya ziara ya kumtembelea Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Doto Mashaka Biteko katika ofisi za wizara zilizopo jijini Dar-es-Salaam.

Ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Tanzania ulioongozwa na Amiri na Mbashiri Mkuu ulijumuiya wajumbe muhimu ambao ni Naibu Amiri wa Mahubiri na Malezi Maulana Abdur rahman Muhammad Ame, Naibu Amiri wa Pili Maulana Abid Mahmood Bhutt ambaye ni Mwalimu Mkuu wa Jamia Ahmadiyya Tanzania, Dkt Saleh Kitabu Pazi ambaye ni Sadir Answarullah Tanzania pamoja na viongozi muhimu wawili wa Majlis Amla taifa katika maswala haya ambao ni Bwana Abdillah Kombo Katibu wa mambo ya nje, na Katibu wa mambo ya ndani ambaye ni Bwana Yahya Yusuf Kambaulaya

Mkutano huu ulikuwa na dhumuni la kwenda kumpongeza kwa kuchaguliwa kwake katika wadhfa huo mpya, na pia kumtambulisha kuhusu kazi za Jamat Ahmadiyya Tanzania pamoja na maendeleo yake katika huduma zake za kiroho na kijamii, kwani sio mara ya kwanza ujumbe wa jumuiya kukutana naye. Pamoja na hayo yote dhumuni kubwa ilikuwa ni kumualika kuhudhuria Jalsa Salana Tanzania 2023, ambapo alitoa jibu la moja kwa moja kuwa hatoweza kuhudhuria lakini atatuma muakilisha, ndipo alimtuma Mhe. **Abdallah Hamis Ulega Waziri wa Mifugo na Uvuvi** kama muwakilishi wake katika Jalsa Salana Tanzania mwaka huu.

Amiri na Mbashiri Mkuu aliutambulisha ujumbe alioambatana nao na baada ya hapo Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu alipata fursa ya kutambulishwa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya na shughuli zake za kiimani nchini pamoja na mchango wake katika maendeleo ya nchi.

Kikao hicho kilichotawaliwa na fikra chanya kutoka pande zote kilihitimishwa na neno la shukurani kutoka kwa Mhe. Naibu Waziri Mkuu na kuhitimishwa na maombi ya kimya yaliyoongozwa na Amiri na Mbashiri Mkuu Tanzania.

Baada ya hapo Mheshiwa Naibu Waziri Mkuu alipokea zawadi ya kopi ya Qurani tukufu yenye tafsiri ya Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya, pamoja na vitabu vingine vya Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya vyenye mchango mkubwa kiimani na ustawi wa amani duniani.

Baada ya hapo ziliufuatia picha kwa ajili ya kumbukumbu za tukio hili muhimu katika shughuli muhimu za Jamat hasa kutengeneza mahusiano mema na serekali.

Je, Afrika tuko Tayari Kuingoza Dunia ?

Kutoka Uk> 12

wa Afrika tuko tayari ??

Jalsa salana ya 52 Tanzania ya mwaka huu 2023 iliyofanyika tarehe 29 September hadi 01 October ili bahatika kupata baraka ya ugeni tena sio mgeni tu bali ni Aaalimu, Mwanachuoni mkubwa wa kiislamu na mwanamajumui wa Afrika Mauluvi Sheikh Muhammad bin Saleh Mwanachuoni huyu aliyezaliwa pembezoni mwaviunga vya mji mtakatifu wa Makka baba yake na mama yake walipo kwenda katika mji huo kufanya ibada tukufa ya hija baada ya kukaa huko kwa muda wa zaidi ya mwaka mmoja ndipo alipo zaliwa Mwanamajumui na mtoto huyu wa Mama Afrika hivi karibuni alishiriki Jalsa Salana yetu ya Tanzania kwakweli hakufanya ajizi aondoke bila kutukumbusha juu ya kufanya maandalizi makubwa kwa sisi na vizazi vyetu juu ya majukumu yaliomabegani kwetu kwa mama Afrika siku moja itakapo iongoza dunia hakika hadithi hii ndefu na yakuvutia aliyotupatia ilianza kwa makaribisho aliyopewa na Kipenzi cheti na Amir na mbashiri mkuu wa Tanzania Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry alipomkaribisha mwana huyu wa Afrika atoe salamu zake kwa ndugu zake wa Tanzania. Mheshimiwa Amir sahib wa Ghana Mauluvi Sheikh Muhammad bin Saleh kwa unyenyekevu mkubwa alianza kutoa maamkizi kama ilivyo ada ya Assalamu alaikum warhmatullah wabarakatuh akasema nimeambiwa nieleze kitu kuhusu nchi yangu ya Ghana na Jamaat Ahmadiyya naamini kazi hii ni nzito kwa sababu sijui wapi pakuanzia na wapi pakuishia. Pamoja na yote nawapongezeni kwa mafanikio mazuri ya jalsa salana yenu 52 kwa hatua hii nimepata faraja na kupata picha kuwa kupitia ninyi bendera ya Jamaat Ahmadiyya na Islam itaendelea kupepea zaidi na zaidi katika nchi ya Tanzania. Pamoja na mafanikio haya mazuri kwa hakika muhesabu kuwa hii ni hatua ya mwanzo tu katika kuyaelekea mafanikio kwani huko Ghana Jalsa salana ya mwaka huu mahudhurio ya ndugu zenu ni zaidi 40,000. Wakati watu wengine wakilibeza bara la Afrika mwanamajumui huyu na Mtoto mwema wa Afrika Mauluvi Sheikh Muhammad bin Saleh alianza kujenga hoja yake kwa kulivika joho la heshima bara hili la Afrika anasema *"Afrika inayo heshima maalumu na wajibu mkubwa mbele ya Mwenyezi Mungu, Afrika imethibitika kisanyansi ndio chanzo cha uhai Afrika inasemekana kisanyansi ni katikati ya dunia, Afrika inatarajiwa kuwa ndio itakuwa kituo na chemchem na kitovu cha maendeleo ya dini tukufu ya Islam "* Hadharat Mirza Bashiruddin Ahmadi ra Khalifatul masih II alipata kueleza kuwa mabara yote yamepata nafasi ya kuingoza dunia kama Asia ,Urusi na Ulaya na Sasa bara la Amerika na alitabiri kuwa baada ya sasa zamu hii zamu inayofata itafika kuwa ni ya Afrika kuiongoza dunia kwa maana ya (Super Power) kwa hakika anahoji leo tusemapo maneno haya mtu anaweza kuona kichekesho kwa kujiangalia tunaweza kujiona watu wanyonge,masikini juu ya utabiri huu Mwanamajumui huyu anahoji je hatukumbuki utabiri wa Mtukufu Mtume mtukufu Muhammad (saw) kuwa Islamu itakuja kuiongoza dunia haya maneno wakiambiwa watu wachache wanyonge na masikini na dhalili kama Hadhrat Bilali ra kuwa iko siku mtaiongoza dunia na kuvaa bangili ya mfalme kisra kama ishara ya ushindi wa dini tukufu ya Islam Jibu lipowazi wakati ulifika na utabiri ulitimia na dini tukufu ya Islamu Iliiongoza dunia. Utabiri unaiweka Afrika katika nafasi maalumu wakati wa zama za pili za ushindi Islamu hakika wakati huo ni zamu za mfuasi wa mtukufu Mtume Mtukufu Muhammad (saw) ambaye ni Hadharat Mirza Ghulam Ahmadi[as] Afrika itaiongoza dunia na wakati huo Islamu itakua na shani maalum. Mwanamajumui huyu wa Afrika anaseme napenda muelewa kuwa mambo haya mawili ya ushindi wa Islamu na Ushindi wa Afrika yameunganishwa pamoja. Iwapo Afrika itafanywa kuwa na nguvu na Islamu itakua yenye nguvu jambo la kujiuliza sisi waafrika ni lipi jukumu letu?. Allah alimuahidi Hadharat Mirza Ghulam

UK. 11

Bustani ya Washairi

ANSARI JITAHIDI.

Kwa jina la Rahmani, hapa mwanzo na mwishoni,
Na Ansari karibuni, Bungu tuna wapendeni,
Twataka yenu maoni, mtuweke elimuni,
Ansari jitahidi, siku zenda ukingoni.

Hii leo siku gani, tuliomo humu ndani,
Tumekuja fanya nini, kujaa msikitini,
Lengo waja wa manani, tukumbushane ya dini,
Ansari jitahidi, siku zenda ukingoni.

Sote tumo safarini, nawambia ikhiwani,
Roho hupaa mbinguni, mwili huenda ardhini,
Ansari sikieni, tuisome kur'ani,
Ansari jitahidi, siku zenda ukingoni.

Wasaidizi ni nani, Ansari nambieni,
Wakajibu waumini, ni sisi ansarini,
Na Isa[as] akabaini, wameshinda mtihani,
Ansari jitahidi, siku zenda ukingoni.

Kweli tujitahidini, muhimili wa nyumbani,
Kwa malezi ya kidini, wana wasiwe wahuni,
Kuna kesi kiamani, taenda kujibu nini?
Ansari jitahidi, siku zenda ukingoni.

Tufate yetu Imani, Islam ndio dini,
Masihi huyu jamani, kaletwa na Rahamani,
Utii tusiwe duni, Ansari ni namba wani,
Ansari jiatahidi, siku zenda ukingoni.

Ahmadi mhisani, ni nyota ya ardhini ,
Huruma toka mbinguni, dini ilikuwa duni,
Walimwengu duniani, waliruka mpakani,
Ansari jitahidi, siku zenda ukingoni.

Ulie Ahmadini, nyota umeibaini,
Umefiti utumeni, kwa vile una Yakini,
Umeridhi ya mbinguni, Nabii huyu fateni,
Ansari jitahidi, siku zenda ukingoni.

Kufikia uzeeni, mara saba usabini,
Mtolee shukurani, muumba wako mbinguni,
Saidia masikini, jitolee kila fani,
Ansari jitahidi, siku zenda ukingoni.

Amka usingizini, kasimame mkekani,
Amsha waamsheni, walo bado vitandani,
Ansari usukani, na ndiwe dira Kayani,
Ansari jitahidi, siku zenda ukingoni.

Siku zenda ukingoni, sikia yangu maoni,
Hujui tarudi lini, kuingia kaburini,
Swali umefanya nini, lipokuwa duniani,
Ansari jitahidi, siku zenda ukingoni.

Kumi na mbili betini, kalamu naweka chini,
Sijaishiwa kichwani, bali muda nasaini,
Tutaonana mwakani, inshalla na kwaherini,
Siku zenda ukingoni, tujitahidi Ansari.

S. Kinywelo [SAMU NKUNGU].

NYWELE

Rabbi alinipa nywele, nyeusi tena za singa
Nambie wazungu pule, wahenga na manyakanga
Ziko wapi nywele zile, zilonifanya kuringa
Na vipi nitazipata, niringe kama zamani?

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani, Migombani.

Kila Ujenzi si nyumba.

Ijilisi nakuomba, hapa ni nyumbani petu
Uketi nami sambamba, tushufu shughuli zetu
Shughuli zenyewe kwamba, juu ya ujenzi wetu
Mwingine wa mafukutu, kila ujenzi si nyumba.

Hatunguza kila kitu, kwa unene na wembamba
Nimekigundua kitu, kitu chenyewe kasumba
Kwayo siketi sukutu, machache hayakuamba
Kila ujenzi si nyumba, mwingine wa mafukutu.

Mwingine wa mafukutu, kila ujenzi si nyumba
Nakuapia baratu, nimeona sijapamba
Dunia pamwe na watu, Allah alituumba
Kila ujenzi si nyumba, mwingine wa mafukutu.

Usiione boritu, vizuri wameiremba
Mataa ya rangi tatu, mweku mweku kila chumba
Laili huwa misitu, na machaka yalofumba
Kila ujenzi si nyumba, mwingine wa mafukutu.

Ujenzi huu mjomba, si salama sisi kwetu
SI nyumba za kujigamba, nasema si mali kitu
Sio mito kuna mamba, pia wamejaa chatu!
Mwingine wa mafukutu, kila ujenzi si nyumba.

Al-Usatadh Mhenga
Khamisi S. S. Wamwela
Mbagala, Dar es Salaam.

MLINDE ZAFRULLAHI

Kwa jina lilotukuka, awali Bismillahi
Mno Umetakasika, hakuna yako shabibi
Mbele yako twaanguka, twakuomba ya llahi
Mlinde Zafrullahi, na Mariamu Swidiga

Dunia mengi mashaka, vijana kutaka wahi
Wazazi wahuzunika, wapi wafiche wajihi
Sisi tumesitirika, twashukuru ya llahi
Muoze Zafrullahi, kwa Mariamu Swidika

Kweli tumefurahika, mwana hajatufedhehi
Mola wajaze Baraka, twakuomba ya llahi
Walindwe na Malaika, Wasibaki majeruhi
Mlee Zafrullahi, na Mariamu Swidika

Watembee kwa haraka, kufata njia sahihi
Sala, saumu na zaka, wazitende kwa fikihi
Na udugu kuushika, katu wasiukebehi
Mkuze Zafrullahi, na Mariamu Swidika

Vazi Ulilowavika, kulivuwa wasiwahi
Usiku wakiamka, wakusujudu llahi
Waongee na kucheka, lugha kwa Istilahi
Atoshe Zafrullahi, kwa Mariamu Swidika

Wadumu kukumbuka, jioni na asubuhi
Waitikie Labeka, kumsikiza Masihi
Wajaze Zako fanaka, wape kizazi swalihi
Mjazi Zafrullahi, na Mariamu Swidika

Mola wangu msifika, mja wako uniwahi
Kwa dhati ninatamka, Alhamdulillahi
Nakuomba Kuitika. Ya Allah Ya llahi
Hafiz Zafrullahi, na Mariamu Swidiga

Abdul-Rahman Muhammad Ame
Dar es Salaam

Kasida ya kumsifu Mtume Muhammad[saw]

...Kutoka toleo lililopita

25

شيئان كان القوم عمياً فيهما حسو العقار و كثرة النسوان

Tafsiri: Watu walikuwa wamepofuka katika maovu mawili; kunywa pombe na (kuoa) wanawake wengi

Maelezo: Kabla ya ujio wa Uislamu watu wengi walizama katika upendo wa dunia na kwenda mbali na dini. Ingawa waliona kwa macho yao ya kimwili lakini walikuwa vipofu kwa macho yao ya kiroho. Pombe ilikuwa sehemu ya lazima ya maisha yao na walichukulia kama mchezo kuoa na kuachana na wanawake. Dini ya Uislamu ikaleta ustarabu kati yao.

Shahabu Ahmad
Morogoro

KASIDA

...Kutoka toleo lililopita

16. نَهَبَ اللِّئَامُ نُشُوْ بَهُمْ وَ عِقَارَ هُمْ
فَتَهَلَّلُوْا بِجَوَاهِرِ الْفُرْقَانِ

Waovu walipora mali zao na miliki zao. Lakini wakachangamka kwa kupata lulu za Kurani.

17. كَسَحُوْا بُيُوْتَ نُفُوْسِهِمْ وَ تَبَادَرُوْا
لِتَمَتُّعِ الْاِيْقَانِ وَالْاِيْمَانِ

Wakafagilia mbali taka za undani wa nafsi zao na wakaharakia kunufaika na yakini na imani.

18. قَامُوْا بِاِقْدَامِ الرَّسُوْلِ بِغَزْوِهِمْ
كَالْعَاشِقِ الْمَشْغُوْفِ فِي الْمِيْدَانِ

Pamoja na Mtume[saw] kusonga mbele, wakasimama kidete kwenye vita vyao katika medani kama ashiki aliyelewa na mahaba.

19. فَدَمُ الرِّجَالِ لِصِدْقِهِمْ فِي حُبِّهِمْ
تَحْتَ السُّيُوْفِ اُرِيْقَ كَالْقُرْبَانِ

Basi damu za nguli, kwa uthabiti wao katika huba yao, zilimwagwa chini ya panga kama dhabihu.

20. جَاءُوْكَ مَنْهُوْبِيْنَ كَالْعُرْيَانِ
فَسَتَرْتَهُمْ بِمَلَاحِفِ الْاِيْمَانِ

Wakakujia kama rabana wakiishaporwa mali yao, nawe ukawavisha shuka za imani.

Kitabu cha KASIDA

Upendo

Mwanaume mmoja alimuoa mwanamke mrembo. Alikuwa akimpenda sana. Siku moja mwanamke alipatwa na maradhi ya ngozi. Kidogokidogo alianza kupoteza urembo wake.

Mume alipata safari na wakati akirudi alipata ajali iliyomfanya apoteze uwezo wake wa kuona. Hata hivyo, maisha yao ya ndoa yaliendelea kama kawaida. Lakini kadiri siku zilivyosonga mbele ndivyo mke alivyoendelea kupoteza urembo wake. Kwa kuwa mume alikuwa kipofu hakulijua hilo na hivyo hakuna kilichobadilika kwenye upendo wao. Aliendelea kumpenda, na mke alimpenda sana mumewe.

Siku moja mke alifariki dunia. Ilikuwa huzuni kubwa sana kwa mume.

Baada ya kumaliza taratibu zote za maziko, mazishi na kutandua msiba, alipanga kuhama kwenye mji huo na kwenda kuishi kwenye mji mwingine.

Mtu mmoja aliposikia habari hiyo alimwendea na kumuuliza: ?Sasa utawezaje kutembea peke yako? Maana siku zote hizi mkeo alikuwa akikusaidia kukuonesha njia.?

Akajibu: Mimi si kipofu. Nilifanya ionekane hivyo kwa sababu angejua kwamba ninauona mwili wake ulivyobadilika kuwa mbaya angepata maumivu makubwa zaidi kuliko ugonjwa wake wenyewe. Alikuwa mke mwema sana. Nilitaka aendelee kuwa na furaha.

FUNZO:

Wakati fulani ni vizuri ukajifanya kipofu na kuyapuuza mapungufu ya mwenzako ili kumfanya awe mwenye furaha .

Meno huung?ata ulimi mara nyingi, lakini vinaendelea kuishi pamoja kinywani. Huo ndio moyo wa KUSAMEHEANA. Macho hayaonani, lakini yanatazama na kuona vitu kwa pamoja, hupepesa na kulia pamoja. Huo unaitwa UMOJA.

Ukiwa peke yako unaweza kuongea, lakini ukiwa pamoja na mwenzako mnaweza KUZUNGUMZA.

Ukiwa peke yako unaweza KUFURAHI, lakini ukiwa na mwenzako unaweza KUFURAHIA

Ukiwa peke yako unaweza KUTABASAMU, lakini ukiwa na mwenzako mnaweza KUCHEKA.

tazama nakumbuka kuwa Kiwembe kina ukali lakini hakiwezi kukata mti; shoka lina nguvu na imara lakini haliwezi kukata nywele hivyo vyote kiwembe na shoka vina umuhimu wake kwa mahala pake

Kila mtu ni muhimu kulingana na kusudio na lengo la uwepo wake. Usimdharau mtu yeyote kwa hali yoyote, kwa sababu huwezi kuwa yeye kwa vyovyote na pia amini kuwa upo umuhimu wa uwepo wake .

Mwenyezi Mungu atujaalie nguvu na moyo wa kusamehe, kustahimiliana na kuishi kwa umoja na upendo .

Kwaheri Mpambanaji, Adam Mpambije.

Na. Mahmood Hamsin Mubiru.

Baadhi ya falsafa tunazisikia na kuzisoma vitabuni. Moja ya falsafa inayotawala katika riwaya, mashairi, mafunzo ya dini ni ile ya kutembea katika ardhi na kutafuta riziki. Na katika kufanya hivyo mawazo yako, fikra zako, matumaini yako, vyote hivyo uviweke mikononi mwa Allah. Ukishafanya hivyo pambana. Jitume. Jaribu. Usitazame nyuma. Usikate tamaa, kama asemavyo Togore yule mshairi maarufu wa India. ***Mlango mmoja ukiwa umefungwa, bisha hodi mwingine***. Hayo yote kwa baadhi yetu ilibaki ni nadharia, maneno matamu lakini kwa Adam Mpambije hayo ndiyo yaliyotawala maisha yake yote. Na hivyo kutuachia somo kubwa. Sisi ni wa Allah na kwake tutarejea.



Adam Mpambije ni mfano wa kijana aliyeshika Imani yake kwa mikono miwili na kuithamini. Uwezekano wa kijana kuingia Afrika ya Kusini akakaa kimya bila ya kubisha hodi kwenye Jumuiya ya Ahmadiyya ulikuwepo. Hakufanya hivyo. Malezi mema aliyoyapata nyumbani yamechangia katika kuendelea kushika kamba hiyo ambayo kila aishikaye hawezi kuanguka. Ushiriki wake katika shughuli za Jamati huko Afrika ya Kusini ni muendelezo wa kutimiza ahadi ya Baiat ya kwamba nitaitanguliza dini mbele ya dunia. Huu ni mtihani mkubwa tunaopambana nao hivi leo. Tunalo la kujifunza kutoka kwa Adam Mpambije ambaye kwa kiwango yeye aliushinda.

Sifa moja kubwa ambayo nimeisikia kwa wengi ni kwamba Adam Mpambije alikuwa Mpambanaji. Nakubaliana nao. Adam aliamini sana katika kile alichokuwa anakitafuta na katika kufikia shabaha hiyo aliweza kupanda milima na kuvuka mito. Nilipata bahati ya kuona jazba ya Adam Mpambije wakati akiwa na kijana wangu walivyopambana kupata elimu ya Sekondari. Nakumbuka juhudi kubwa aliyoifanya Mussa Mpinga Sahib katika kukamilisha ndoto hii ya Adam Mpambije kupata elimu. Yalikuwa ni mapambano kweli kweli. Nakumbuka Adam Mpambije akianzisha kituo cha kufundisha kiingereza pale Temeke. Pale ambapo uliona haiwezekani hapo hapo ndipo alipopita na kukuonesha kwa vitendo kwamba ulikosea. Na baadae nilipopata taarifa zake. Zilikuwa ni juu ya mapambano ya kwenda mbele. Aliamini juu ya msaada wa Allah na kuendelea kupambana.

Vijana wetu wanasomo katika maisha ya Adam Mpambije. Vijana wetu watoke. Wachangamke. Wajitume. Maendeleo tunayoyaona duniani vijana walitoka. Wakajituma. Wakapambana na matatizo. Na waliondoka bila chochote. Ndiyo hisitoria ya Marekani hivi leo. Vijana wetu wasikate tamaa. Wapambane. Roma haikujengwa siku moja. Wapo vijana wenye shauku na jazba ya kutafuta. Tuwaelimishe. Tuwaelekeze. Tuwashauri. Kutafuta si kosa bali ni Ibada. Tuwape moyo. Tuwape msaada. Maendeleo yao yamefungamana na maendeleo yetu. Hiyo ndiyo ilikuwa ndoto ya Adam Mpambije, kwa msaada wa Allah tunaweza kuitimiza ndoto hiyo, kwa vijana wetu. Na daima kuendelea kumuombea Adam Mpambije.

Dua tunamuombea, kijana wetu Adamu
Twaomba kumpokea, Yarabi Mola Karimu
Makosa kumfutia, apate pepo naimu
Wapewayo waja wema, wema walio ongoka.

Kuiendea Elimu na matumizi yake yenye Baraka kwa mujibu wa Islam

Na. Swaleh Kitabu Pazi

Bismillah Rahman Rahim
Asalaam Alaykum
Warhmatullah Wabarakatuh.

Waheshimiwa Amir Jamaat Tz, Ghana.

Waheshimiwa Naib Umaraa

Masheikh na Wajumbe wa Majlis Amila wote

Wanajamaat wote mliohudhuria Jalsa Salana Tz 2023

Mada:

Kuiendea Elimu na matumizi yake yenye Baraka kwa mujibu wa Islam.

Kuiendea elimu na matumizi yake yenye Baraka kwa mujibu wa Islam, ndiyo mada niliyotumwa kuizungumzia mbele ya kadamnasi hii. Awali ya yote, yanipasa kutanguliza maombi ya unyenyekevu mbele ya Allah ambaye hukisemesha kila kiumbe, ili anitanulie kifua changu na anifungulie kifungo ulimini mwangu, niweze kunena yale yatakayopenya akilini mwa wasikizi wangu.

Kuiendea elimu, siyo tu kwamba ni jukumu muhimu katika maisha ya kila mmoja wetu, bali ni jihadi takatifu ipaswayo kufanywa na kila muislam katika maisha yake ya kila siku. Mtume Mtukufu saw aliwahi kukaririwa akisema;

Twalabul 'ilmi fariidwatun 'alaa kulli muslim wa muslimah

Kutafuta elimu ni faradhi ya kila muislam wa kiume na wa kike.

Hivyo kwa mujibu wa kauli hii ya Mtukufu wa daraja, saw, ni kwamba kuiendea elimu yapaswa kuwa ni safari muhimu katika nyendo za kila siku katika maisha yetu. Hapa tunafundishwa ya kuwa maisha ya muumini hayatengani na utafutaji wa elimu kwa namna yoyote ile. Baadhi ya wana falsafa hudai kuwa elimu ndilo jambo pekee lililomtenganisha mwanadamu kutoka katika kundi la wanyama.

Katika baadhi ya nadharia za kisiasa husemwa kuwa kazi ni kipimo cha utu.
Lakini mbele ya wana falsafa kipimo hasa cha utu ni elimu, na hii hasa ndiyo nadharia itokanayo na mafundisho ya Islam.

Katika mafundisho ya Qur'ani Tukufu inabainishwa kwamba kusudi kuu la kuumbwa kwa watu na majini ni kumwabudu Mola wao, Allah Anasema;

Wa maa khalaqtul jinna wal insa illa liya'buduun. Na sikuumba watu na majini isipokuwa waniabudu (51:57).
Ibada ndiyo msingi mkuu wa kuumbwa kwetu, na mojawapo ya tafsiri ya neno ibada ni kuiga na kujiambukiza sifa za Allah. ili kuziiga sifa hizo kuna ulazima mkubwa juu ya utambuzi wa sifa hizo, ambao bila shaka ndicho kile kiitwacho elimu. Ni katika kuthibitisha nadharia hii ndiyo maana Allah Anatubainishia ndani ya Qur'ani Tukufu; Innamaa yakhshallaahu min 'ibaadihil 'ulamaa-u.

Hakika wanaomcha Allah katika waja wake ni wenye elimu (35:29)

Jambo la kupendeza zaidi ni kwamba nadharia hii inapatikana katika mafundisho ya Islam pekee. Kabla ya Islam, elimu aghalabu ilihesabiwa kuwa ni pingamizi kuu dhidi ya imani za kidini. Ukweli huu unathibitika pale tunaposoma taarifa za wasomi mbali mbali kutengwa na nidhamu za kidini, kuteswa na hata baadhi yao kuuawa kutokana na fatwa zao za kielimu kuhesabiwa kuwa zinapingana na maelezo ya kimbingu.

Mwaka 399 BC, Socrates, mtu aliyeaminika kuwa msomi kuliko mtu yeyote duniani, alishitakiwa kwa kuvuruga mawazo ya vijana wa Athens na kuikufuru miungu ya kigiriki. Mashitaka haya yalitokana na Socrates kuibatilisha imani ya miungu hiyo kwa hoja nzito za kielimu. Wakati wa kesi yake, Socrates alijaribu kujitetea kwa hoja nyingi zenye nguvu, lakini waumini wa upagani wa kigiriki hawakumwelewa hata kidogo. Heshima pekee aliyopewa ilikuwa ni kutakiwa tu ajichagulie aina ya kifo chake. Sokrates alichagua auawe kwa kunywa sumu, na siku ya kifo chake alipewa kikombe cha sumu itokanayo na mmea, iitwayo **hemlock**.

Hata Aristotle, msomi mwingine aliyeibuka baada yake, alikufurishwa na uma wa wafuasi wa dini ya kiathenia. Akitajwa kama mtu aliyekufuru na kukosa uchamungu na adhabu ile ile iliyotolewa kwa Socrates ilipendekezwa dhidi yake.
Lakini huyu hakusubiri auawe, alipobaini tetesi za kuwindwa kwake alitoroka kutoka Athens na kukimbilia katika kisiwa cha Euboea na kujificha huko hadi mwisho wa uhai wake.

Mwezi Machi mwaka 415 AD, katika mji wa Alexandria uliokuwa kiini cha wasomi katika dola ya kirumi, mwana falsafa wa kike aliyeitwa Hypathia, aliuawa na kundi la wauaji wa kikristo waliotumwa na Askofu mkuu wa mji huo.
Hii ilitokana na baadhi ya maoni yake, yaliyopingana na itikadi ya kanisa kuwavutia hata baadhi ya mapadri wa kikatoliki. Pia tunasoma juu ya kutengwa kwa wana sayansi kama Nicolas Corpenicus na Galileo Galilei katika karne ya 15 na 16. Kadhalika tunasoma kumhusu mwana hisabati, mwana fizikia na mnajimu wa kiingereza wa karne ya 17, Isaac Newton, aliyetengwa na kanisa baada ya kueleza kuwa hisabati zake zinakataana kabisa na dhana ya utatumtakatifu, usiogawanyika. Alifutwa kazi katika chuo kikuu cha Cambridge na akatengwa na kanisa kutokana na kilichodaiwa kuwa ni uzushi.
Hata katika Uyahudi kuna ushahidi wa kuteswa, kutengwa na hata kuuawa kwa watu wenye elimu kwa sababu za kidini.
Hali hii iliendelea hadi kwenye karne ya 17, pale mwana falsafa maarufu wa kiyahudi, mzaliwa wa Ureno, Baruch Spinoza, alipokufurishwa. Alifukuzwa kwenye dini na wakuu wa dini ya kiyahudi akiwa na umri wa miaka 23 tu. Ilidaiwa kuwa nadharia zake nyingi zilikuwa zikipotosha kuhusiana na usahihi wa maandiko yao ya dini, Taurati na Talmudi.

Hivyo ni katika Islam ndiko elimu ilikopewa chumba cha heshima na utukufu. Ni kana kwamba elimu ilikuwa ni sehemu muhimu mno ya ujumbe wa Mtukufu Mtume, Muhammad saw. Mafundisho yenyewe ya Islam yameitwa Elimu kwa kauli ya Allah, Aliyemwambia mtume wake kwamba;
Wala init taba'ta ahwaa-ahum ba'dal ladhii jaa-aka minal 'ilmi, innaka idhanl laminadhw dhwaalimiin.

Na kama ukiyafuata matamanio yao baada ya kukufikia elimu, hakika hapo utakuwa miongoni mwa wadhalimu (2:146).

Elimu inayotajwa hapa kuwa imemfikia Mtume saw, haikuwa ujuzi wa kusoma na kuandika, kuhesabu na kuchora au kushona na kudarizi. Bali ilikuwa ni mafundisho ya dini yaliyoletwa na Allah kwa njia ya ufunuo, ambayo kwa hakika ndiyo elimu halisi na ya kweli.
Bali mafundisho hayo ndiyo chemchem ya elimu zote ambazo mwanadamu huzitafuta kila uchao. Bila shaka maana halisi ya elimu ni utambuzi, na utambuzi wa kweli ndiyo unaoweza kuitwa elimu sahihi. Kwa mujibu wa lugha ya kiingereza, elimu huwakilishwa na neno knowledge, ambalo huainishwa kwa maana zifuatazo; facts, information, and skills acquired through experience or education. (uhalisia, taarifa, na weledi upatikanao kupitia uzoefu au mafunzo).

Kupitia ainisho hili tunaweza kubaini kuwa kuiendea elimu ni jambo linalopaswa kuambatana na jihadi kubwa ya kujifunza na kutafiti kila jambo tunalohitaji

kulijua. Hatua hii kamwe haiwezi kufikiwa kwa juhudi pekee za kibinadamu, bali ni lazima ziambatane na msaada wa Allah. Na kwa upande mwingine, msaada huo wa Allah haushuki mahala pasipotanguliwa na jitihadi. Hii ni kanuni iliyowekwa na Allah, iliyotangazwa kupitia Qur'ani Tukufu kwamba;

Wal ladhiina jaahaduu fiinaa lanahadiyannahum subulanaa, wa innal laaha lama'al muhsiniina.

Na wale wanaojitahidi kwa ajili Yetu, kwa yakini Tunawaongoza katika njia zetu.
Na bila shaka Allah Yu pamoja na wafanyao wema. (29:70).

Hivyo katika kuliendea kila jambo, juhudi inapaswa kutangulia ili kuvuta msaada wa Allah katika ufanikishaji wa jambo husika. Hadhrat Muslih Mauud ra, akielezea juu ya kudura za Allah, alisema kuwa katika kanuni za uwezo wa kiungu kuna tadbiir na taqdiir. Tadbiir ndio ile juhudi ya kibinadamu, na taqdiir ndiyo kudura ya Allah, ambayo bila shaka hujitokeza pindi tadbiir

Itaendelea..... toleo lijalo Inshallah

MATUKIO KATIKA PICHA









Njia ya Kulinda Maadili Mema katika Taifa

Kutoka uk. 1

Na Rajabu Abasi Mkieti
Kitonga –Dar es Salaam

Hayo yamesemwa na Amir na Mbashiri mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Amadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akitoa hutuba ya kufunga Jalsa salana ya 52 ya mwaka 2023 iliyofanyika katika mkoa wa Dar es salaam wilaya ya Ilala kata ya msongola kitonga ambayo ilifanyika kuanzia tarehe 29 mwezi September mpaka 1 October 2023. Amir sahib akifunga Jalsa Salana alieleza kuwa maisha ya Mtukufu Mtume mtukufu Muhammad (saw) yalikua ni tunu na darasa la namna ya kipekee katika kulinda haki na kukuza maadili katika taifa kwani huwezi kusema leo unalinda haki za watu na viumbe wengine kama hustawishi maadili mema katika jamii kwa kupitia mafundisho ya dini tukufu ya islamu, akiendelea kueleza Amir sahib alimnukuu mara nyingi zaidi Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Amadiyya Hadharat Mirza Ghulam Ahmad as katika maandishi yake kwa namna alivyoeleza maisha ya mtukufu Mtume mtukufu Muhammad (saw) yanavyo weza kubadili tabia ya watu katika taifa hadi kuwafikisha katika kilele cha wema wa maadili na hali kuishi katika maingiliano na watu wa dini tofauti. Akimnukuu Hadharat Mirza Ghulam Ahmad as anasema kuihusu jumuiya hii kuwa " *Zama hizi pia ni za vita vya kiroho. Vita na shetani vimeanza. Shetani anaishambulia ngome ya Islamu kwa silaha na hila zake zote na anataka kuishinda Islamu, lakini Mwenyezi Mungu Ameanzisha silsila hii kwa wakati huu ili kumshinda Shetani milele katika vita vya mwisho''malfudhati* . Maendeleo ya mwanadamu hayawezi kuyaepuka mapinduzi makubwa ya kiroho aliyoyaleta Mtume Muhammad saw. Amir sahib alieleza zaidi kuhusu mada hiyo kwa kunukuu Hadharat Mirza Ghulam Ahmad as aliyesema *''Hizo zilikuwa ni dua za mausiku yenye kiza za mja aliyejipoteza ndani ya Mungu"Lile tukio la ajabu lililotukia katika nchi ya jangwa la Arabuni kwamba malaki ya watu wakahuika katika siku chache, na waliokuwa wameharibika tangu vizazi hadi vizazi wakazishika khulka za Mungu, na vipofu wakaanza kuona, na midomo ya mabubu ikaanza kueleza maarifa ya Mungu, na mara moja mapinduzi yale yakapatikana duniani ambayo hakuna jicho lolote lililoyaona hapo kabla , wala sikio lolote lililoyasikia. Mwafahamu hiyo u ambazo zikapaza vilio duniani na zikaonyesha maajabu yaliyoonekana hayawezekani kwa yule asiye na msaidizi, asiyejua kusoma na kuandika. E Mungu, Umrehemu na umpe amani na Umbariki yeye na ali zake kiasi cha hamu yake na ghamu yake na huzuni yake kwa ummati huu, na Umteremshie nuru za rehema Yako hadi milele."* Amir sahib alisema madai yetu ya takuwa bure kama hatuta ambatanisha vitendo vyema katika kuishimaisha yetu na maneno hivyo tukiwa Waahmadiyya tunajukumu la kusema na kutenda sawa sawa na tunayo amini hii itakua njia bora katika kuokoa jamii kutoka katika dimbwi la maasi na machafu kwa kuiga maisha ya Mtume Muhammad saw. Amir sahib alitamatisha hutuba yake kawa kumnukuu muanzilishi wa jumuiya ya Ahmadiyya aliyesema *"Siku zote ogopeni laana ya mungu, kwani yeye ni mtukufu tena mwenye ari. Mwovu hawezi kupata ukaribu kwa mungu, mwenye kiburi pia hawezi kumkaribia, mdhalimu hawezi kumkaribia, haini hawezi kumkaribia, kila asiye na ari kwa jina lake hawezi kumkaribia. Na wale wanaoangukia dunia kama mbwa na sisimizi na mbesi na wanafurahia dunia hawawezi kumkaribia. Kila jicho baya liko mbali naye na kila moyo mchafu hauna habari naye, atakayekuwa katika moto kwa ajili ya mungu, ataokolewa katika moto. Mwenye kulia kwa sababu ya mungu atakuja cheka, na mweney kuacha dunia, atakutana naye. Kuweni wapenzi wa mungu kwa ukweli wa mioyo yenu, na kwa shuku sana, na kwa hamu nyingi ili Mungu pia Awe mpenzi wenu. Rehemuni walio chini yenu na wake zenu na walio maskini katika ndugu zenu, nanyi mtarehemiwa mbinguni vilevile. Kuweni wa mungu kikweli kweli, naye atakuwa wa kwenu. (Al-Wasia)"*. Katika jalsa salana ya mwaka huu tulibarikiwa sana kwani kulibahatika kuhudhuriwa na wagani mbalimbali mawaziri na manaibu waziri pamoja na Amir na mbashiri mkuu wa Ghana wa jamaati Ahmadiyya Ghana kipenzi chetu Maulvi Mohammed Bin Salih nayeye pia alipata bahati ya kueleza mafanikio ya nchi Ghana kwa upande wa jammat Ahmadiyya kwania alisema katika jamaati ya Ghana jalsa salana yao inawahudhuriaji wengi zaidi ya hapa kwa mwaka huu mahudhurio yao ni zaidi ya 40,000 na katika nchi hiyo jamaaati inamiliki shule zaidi ya 400 na huduma mbalimbali zai kijamii ikiwamo hospitali. Katika Jalsa salana ya 52 ya mwaka 2023 mada mbalimbali ziliwasilishwa na wasomi na wataalamu wa jamaati mada hizo ni ***,Jinsi Ukhalifa Unavyoimarisha Maungano yetu na Mwenyezi Mungu*** iliyowasilishwa na Sheikh Tahir Ramadhan Marunda, ***Haja ya Kweli ya Kutangaza Jinsi Maisha ya Mtukufu Mtume (saw) yanavyodhirisha Uwepo wa Mwenyezi Mungu*** Sheikh Shahab Ahmad wa Jamia, ***Kujitolea Mali katika njia ya Allah kunavyokuza Mapenzi ya Mwenyezi Mungu*** Sheikh Abid Mahmood Bhutti wa Jamia, ***Kuiendea Elimu na matumizi yake yenye baraka kwa mujibu wa Islam*** Dr Swaleh Kitabu Pazi, ***Historia ya Ahmadiyyat Tanzania – Mchango wa Lajna Imaillah*** Sheikh Karimuddin Shams, ***Masihi Aliyeahidiwa - Imani yake katika kumtegemea Mwenyezi Mungu*** Sheikh Khawaja Muzaffar Ahmad, ***Maisha ya Ndoa - Mlango wa kumwelekea Mwenyezi Mungu*** Sheikh Abdulrahman Mohammed Ame. Upande wa Banda la maonesho mambo yalikua ya moto moto na ya kuvutia mno kulikua na kitengo maalumu cha Tabligh kwa wageni ambao sio waahmadiyya hali hii ili weza kuwafanya watu 19 kujiunga na jamaat Ahmadiyya kutokana na kazi hiyo kwa kuvutiwa na elimu ya jumuiya ya Ahmadiyya. Mwaka huu Jalsa salana ilibarikiwa na kuhudhuriwa na watu 4070. Mgeni rasmi katika Jalsa Salana ya mwaka huu alikua ni Makamu wa Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dr Philip Mpango ambayea aliwakilishwa na Naibu waziri nchi ofisi ya Makamu wa Raisi (muungano na mazingira) Mh Khamis Hamiza Khamis katika ujembe uliwasilishwa na Naibu waziri ili alisisitiza namana nchi inavyotakiwa kuuenzi umoja na mshirikiano wa kitaifa Mheshimiwa Naibu waziri alisisitiza azidi jamii inavyoweza kutunza na kukuza maadili mema kwa kushirikiana na serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Raisi Dr Samia Suluhu Hasani, Bahati njema katika nyakati tofauti Waziri wa mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Abdallah Ulega naye alibahatika kushirika katika jalsa salana Mh waziri wa mifugo alihamashisha washiriki wa jalsa salana kukimbilia fursa zinzo tolewa na Raisi Dr Samia Suluhu Hasani katika Nyanja ya ufugaji na uvuvi katika sehemu tofauti tofauti Mheshimiwa waziri alisema wizara pia inatoa fursa kuwekeza kwa mtu binfasi, vikundi na kampuni katika ufugaji na uvuvi. Allhamdulilah jalsa salana ilikua ya kipekee kwa kurushwa mubashara kupitia mtandao wa kijamii wa Youtube kwa siku zote tatu

Je, Afrika tuko Tayari Kuingoza Dunia ?

Kutoka uk. 5

Ahmadi as yakuwa *"Mimi nitafikisha ujumbe wako pembe zote za dunia"* bishara hii ya Mashi aliyeaidiwa as kupitia Makhalifa wake waliandaa jeshi maalumu kuja katika bara hili la Afrika kwa lengo hili la kuzagaza ujumbe wa Islamu .Wajibu wetu tutafakari je majukumu yetu ni yapi na tumeyatimiza? Siku zote kazi ya kufikisha ushindi wa dini inahitaji jukumu kubwa la kujitolea kwa hakika kazi hii sio rahisi na haitakua kazi rahisi hata kidogo Mtume Mtukufu Muhammad[saw] pamoja na masahaba wake walijitolea kutokana na upinzani mkubwa wakati huo wakusambaza ujumbe wa Islamu na hata wakati wa Hadharat Mirza Ghulam Ahmadi as pamoja na masahaba zake mengi yamewakuta ikiwamo wale wa zama za nyuma jinsi walivyo jitolea muhanga mali zao heshima zao katika dini tukufu ya islamu hili ni somo tosha kwani tunawaona ndugu zetu wa Pakistani na walioko nje ya Pakstani wanavyojitolea zaidi hali hii inawapa taarifa dunia kuwa ifanye vyovyote lakini ujumbe huu wa Hadharat Mirza Ghulam Ahmadi as hauta kwama katu pia tufahamu na sisi tukitaka tuione bendera ya Ahmadiyya ilipepea katika bara la Afrika basi tuhakikishe tunajitolea muhanga kila kitu kwa kuiambia Dunia na sisi tuko tayari kwa lolote ili bendera ya Ahmadiyya inangara katika dunia. Mauluvi Sheikh Muhammad bin Saleh anasema basi siku itafika ndugu zetu wa Afrika watakapo tuona tunaelekea kwenye kupata ushindi watatuua watatutesa wata tunyanyasa basi tujitayarishe kwa lolote hata kwa kutao damu zetu,kutoa uhai na heshima yetu kwa kuibeba bendera ya Ahmadiyya. Mwanchuona huyu anaendela kusema kuwa mwanajamati yoyote wa Tanzania iwe amejiunga ama amezaliwa na anaishi kwa salama hana changamoto yoyote inayo tokana na kuwa kwakwe Ahmadiyya basi lazima atafakari na ajichunguze ni kweli amesimama kwenye kujitolea na kuitangaza Ahamadiya kwa sababu kwa hakika kama yoyote atasimama kuitetea Ahmadiyya basi atakabiliwa na upinzani na hapo kwa kuushinda upinzani huo basi hapo ndipo tunapo takiwa tujue tumetimiza kiapo chetu cha Ahadi. Mauluvi Sheikh Muhammad bin Saleh akigeukia upande wa kuelezea jamaat Ahmadiyya Ghana anasema mbegu ya kwanza ya Ahmadiyya ilipandwa 1921 kiasi kwamba jammati Ahmadiyya Ghana ina miaka 102. Wakati huko Ghana waliamini Islamu ilikua dini ya watu weusi na wazee wetu katika miaka 1918 kundi moja la waislamu wa Ghana mtu mmoja miongoni mwao alipata njozi kuwa mtu mweupe anaongoza sala basi habari hizo zilifika kwa mtu mfanyabiashara mmoja wa kinaigeria basi bahati njema mfanyabiashara huyo katika bandari ya Saltport bandari ya chumvi basi akasema kuna watu fulani wapo Uingereza hao ni watu weupe na ni waislamu na ninayo nakala ya Gazeti lao la ***Review of Religions*** haya magazeti yanazungumza uislamu. Lile kundi la waislamu walishawishika na kuona wapate anuani ya hao watu ili wawasiliane nao na walimuandikia kionmgozi wa Jumuiya ya Ahmadiyya wakati huo Hadharat Mirza Bashiruddin Ahmadi ra Khalifatul Masih II[ra] wakamuandikia ili awaletee imamu mwaupe na yeye Khalifa akawajibu tumeni pesa tununue tiketi kwanjia ya meli basi wao walichanga na walituma hizo pesa na imamu alitumwa mwaka 1921 alipofika huyo imanu hapo katika bandari ya chumvi basi lile kundi la waislamu lilikuja kumpokea na wao waka mpakia katika mabega yao kama wanavyo fanya kwa wafalme kutokana wakati huo hapa kuwana gari na hawa kumruhusu kutembea kama kilometa 25 kutokana na kuwa mgeni huyo alikua wa thamani sana kwao walipo fika katika mji wao walisalishwa na huyo imamu baada ya sala watu wote walioko pale walijiunga na Jumuiya ya waislamu Ahmadiyya bila hata kupepesa macho. Ndugu hawa walipo jiunga na Ahmadiyya watu katika mji wao walikuja kuwapinga na ndugu hao Ahmadiyya walisimama imara katika kulinda imani yao kwani waliwaambia kuwa watahakikisha mti huu wa Ahmadiyya unapandwa katika kila kijiji cha nchi ya Ghana kwani leo ukifika Ghana Jamaati Ahmadiyya inayo nafasi maalumu na nguvu kwa serikali kwani nchi ya Ghana haiwezi kufanya maamuzi mzito katika nchi bila kupata ushauri kutoka Jamaat Ahmadiyya. Amir sahib Ghana anasema na yeye ni tunda la wazee wale wa mwanzo na baba yake alikua ni moja wa ulamaa wakubwa. Baba yake alifanye mipango kwenda Saudi Arabia ilikufanya hija basi wakati huo yeye aliku haja zaliwa bahati mbaya wakati huo wanafika bandarini meli ilikua imeshaondoka iliokuwa inakwenda hija basi baba yake akakaa huko mpaka mwaka wa pili akaenda kufanya hija hali hiyo ilimfanya yeye kuzaliwa huko Saudia Arabia. Basi baba yake aliporudi hija wajomba zake walikuja kumchukua mama yake kwani walishajua kuwa amejiunga na Ahmadiyya baba yake akawajibu kuwa mchukuweni bint yenu ila huyu mtoto sio wenu na atakaye mgusa atajuta na mama yake alichukuliwa na kupelekwa mbali akiwa bado mtoto na mwezi mmoja . Amir sahib Ghana anasema wakati huo waahmadiyya walizidi kufanyiwa mateso basi baba yake alikwenda kwa utawala wa ukoloni kuomba usalama na walimpa ulinzi wa usalama kwani aliwaambia je kuna mtu mwenye haki ya kuingiliwa katika imani yake na uongozi ukashawishika, baba yake alifanya mahubiri makubwa na yangufu basi baba yake alipokaribia alipofikia karibu ya kufarika aliwaita ndugu zake kuwa mimi nadhani sitaweza kufanikiwa mtoto wangu awe mbashiri basi naomba nikiondoka katika hii dunia mnafanikiSHa tamanio langu la mtoto Wangu anasomea ubashiri basi ndivyo ilivyo tokea alikwenda Rabwah kusoma ubashiri na aliporudi ndio wakati alipo kutana na mama yake mzazi. Amir Sahib Ghana anasema katika nchi ya Ghana leo kama matunda ya kujitolea kwa wazee wao wa Ghana kama utawauliza kundi la watu maarufu Ghana basi huwezi kosa jina lake bali si yeye bali ni Amir wa Jamaati Ahmadiyya Ghana, anaendelea kueleza kuwa katika nchi ya Ghana katika mji ule waliofanyiwa mateso wazee wao kutokana na matesao hayo viongozo wakuu wa vyama vyenye nguvu katika nchi ya Ghana wanatoka katika mji huo hata wakihesabiwa watu matajiri ni waahmadiyya anasema hayo sio fahari bali tuone ni kwa namna gani kujitolea katika dini kutakavyo badili maisha ya vizazi vyetu haraka. Amir Sahib Ghana anasema katika nchi hiyo Amir sahib Ghana anaheshima ya ubalozi serikali inatambua hilo na katika jamaati ya Ghana inamiliki shule zaidi ya 400. Mwisho Amir sahib Ghana anasema kutokana kujitolea kwa wazee wao hivi karibuni katika uchaguzi wa nchi uliopita hiyo wagombea wawili wa urasi wenye nguvu walikua wakimtafuta Amir sahib Ahmadiyya Ghana kumwambia awaombee asubuhi alfajir wakati akiwa yuko katika maandalizi ya sala ya alfajir mara mgombea mmoja wapo wa urasi alimpigia simu kuwa niombee basiakamwambia nakuombea basi mara alipokua amesha maliza kusali na anakwenda kushiriki katika uchaguzi mara akaitwa na mke wake kuwa simu inaita kumbe mgombe mwingine wa uraisi chama kingine naye akamwambia matumaini ya ushindi wangu katika uchaguzi yapo katika maombi yako anasema hii ndio hali ya Ghana. Amasema sio kwa sababu yanafanywa kwa sababu yeye Mauluvi Sheikh Muhammad bin Saleh bali ni kwa sababu ya heshima ya jumuiya ya Ahmadiyaa. Mauluvi Sheikh Muhammad bin Saleh. Mwanamajumuhi huyu anasema jukumu la kiapo chetu ni kuwa tujutahidi kujitolea kwa hali zetu zote na wahakikisheeni haya kuwa yote yatatakea katika nchi hii ya Tanzania InshaAllah. Mauluvi Sheikh Muhammad bin Saleh amemalizia kwa kutuombea kuwa Allah atubariki sote kwa hayo aliyo yasema. Kwa hakika maneno ya mwanamajumui huyu ya na choma kama mshale kwani yanavuta hisia za sisi Waafrika kuhakikisha tunajiweka tayari katika kuiongoza dunia kwa sharti la kuweka mali na heshima zetu katika kuitumikia dini kama sadaka kwa vizazi na jamii nzima ya waafrika.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

HABARI UK> 4

Yesu aliongozwa na nani Nyikani?



HABARI UK> 7

Kwaheri Mpambanaji

Je, Afrika tuko Tayari Kuingoza Dunia ?

Na Rajabu Abasi Mkieti
Kitonga –Dar es Salaam



I firmly believe that if the African countries and people unite together and fulfil the requirements of justice, then one day, Africa will emerge as a true global power. May Allah enable this to happen, InshaAllah (The review of religions January 2012,Vol. 170-ISSUE ONE. Pg 55) Tafrisi isiyo rasmi:- Ninaamini kabisa kwamba ikiwa nchi na watu wa wafrika wataungana pamoja na kutimiza matakwa ya haki siku moja, Afrika itaibuka kama nguvu ya kweli ya ulimwengu. Mwenyezi Mungu awezeshe hili litokee, InshaAllah Ni muongo mmoja sasa tangu Hadharat Mirza Masroor Ahmad atba kiongozi wa jumuia ya waislamu Ahmadiyya duniani kusema maneno hayo lakini swali je watu

UK. 5

Kuiendea Elimu na matumizi yake yenye Baraka kwa mujibu wa Islam

UK. 8

Selected Writings of
The Promised Messiah a.s.
in Kiswahili.



Minaratul Masih - Qadian

BAADHI YA MAANDIKO

YA

HADHRAT MIRZA GHULAM AHMAD (A.S.)

MASIHI ALIYEAHIDIWA NA IMAM MAHDI

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 1,550/=

Je, Wajua?

Je wajua papa Urban VIII katika mwaka 1633 alimhukumu galileo galilei kifungo cha Maisha katika nyumba yake (kifungo cha nyumbani) kwa muda wote wa Maisha yake kwa kosa la kuamini kuwa jua lipo katikati na dunia inazunguka jua. Miaka takribani alfu moja iliyopita, Quran ilinadi kuwa dunia inazunguka jua.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com